

KONGAMANO LA MKUTANO WA ALTA – KIKAO CHA 12

Mada Kuu

**Lugha za Kiafrika na utandawazi:
Changamoto, Matarajio, na Uwezekano**

MWALIKO WA MAKALA YA JOPO LA KISWAHILI

Tunayo furaha kuwatangazia wataalamu, walimu, watafiti, na wapenzi wa Kiswahili kwamba kwa mara nyingine tena tutakuwa na jopo la makala ya Kiswahili kwenye kongamano la mkutano wa ALTA 12 litakalofanyika Chuo Kikuu cha Wisconsin, Madison, kutoka Aprili 24 mpaka Aprili 27, mwaka 2008. Jopo hili litashughulikia ufundishaji wa Kiswahili na lugha za Kiafrika katika muktadha wa mada kuu ya kongamano. Jopo lote litafanyika katika lugha ya Kiswahili

Jopo linakaribisha makala kuhusu vipengele vyovyote vya mada kuu, kama vile: uhusiano baina ya utandawazi na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, utayarishaji wa zana mbali mbali za kufundishia, matumizi ya teknolojia katika kufundisha/kusoma Kiswahili, utahini wa wanafunzi, na kadhalika. Unaweza kupata vipengele vingine kwenye tangazo la kongamano la ALTA:

<http://lang.nalrc.wisc.edu/alta/conf/2008/call2008.htm>

Tafadhali peleka kifupisho cha makala yako, **kisichozidi maneno 500**, kama kiambatisho cha barua-pepe, **Novemba 30 au kabla**, kwa:

Alwiya S. Omar (aomar@indiana.edu)

Zingatia: Kushiriki katika jopo la Kiswahili, hakumzuii mshiriki kuandaa makala ya Kiingereza ya mada tofauti katika majopo mengine ya ALTA na/au NCOLCTL.